**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MAELEZO YA SPIKA KUHUSU MATUKIO MUHIMU KUELEKEA NA WAKATI WA MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE

**OFISI YA BUNGE**
**DODOMA**

## MAELEZO YA SPIKA KUHUSU MATUKIO MUHIMU KUELEKEA NA WAKATI WA MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa mujibu wa Hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuungwa mkono na Bunge, Mkutano ujao wa Bunge yaani Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge utaanza tarehe 08 Aprili, 2025. Kwa kuzingatia hilo, naomba niwape maelezo mafupi kuhusu matukio muhimu kuelekea na wakati wa Mkutano huo kama ifuatavyo:-

(i) Tarehe 10 Machi, 2025 - Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge vitaanza. Aidha, Serikali itawasilisha kwa Katibu wa Bunge Nakala za Dondoo za Vitabu vya Bajeti pamoja na Randama za Makadirio hayo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. [Kanuni ya 115 (1)].

(ii) Tarehe 11 Machi, 2025 - Utafanyika Mkutano wa Wabunge wote ambapo Waziri wa Mipango na Uwekezaji atawasilisha Mapendekezo ya Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Waziri wa Fedha atawasilisha Mapendekezo ya Serikali ya Kiwango na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. [Kanuni 116 (1) na (2);

(iii) Tarehe 12 Machi, 2025 - Kamati za Kudumu za Kisekta zitaanza ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. [Kanuni ya 117 (1)];

(iv) Tarehe 19 Machi, 2025 - Kamati za Kudumu za Kisekta zitaanza uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo. [Kanuni ya 117 (2)].

(v) Tarehe 02 Aprili, 2025 - Vikao vya Mashauriano kati ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali vitaanza kufikiria masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati Kamati zikijadili utekelezaji wa kazi wa Wizara. [Kanuni ya 117 (4), (5) na (6)];

(vi) Tarehe 8 Aprili, 2025 - Mkutano wa Bajeti utaanza rasmi.

(vii) Tarehe 12 Juni, 2025 – Inategemewa Bajeti ya Serikali itasomwa.

(viii) Tarehe 26 Juni, 2025 - Inategemewa Waziri Mkuu atatoa Hotuba ya Kuhitimisha Shughuli za Bunge la Kumi na Mbili;

(ix) Tarehe 27 Juni, 2025 - Inategemewa Mheshimiwa Rais atalihutubia na kulifunga rasmi Bunge la Kumi na Mbili.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kifupi, hayo ndiyo matukio muhimu ambayo tunayarajia wakati tunapohitimisha Bunge la Kumi na Mbili. Nimeyaeleza mapema ili muweze kupanga ratiba zenu vizuri na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu kila mmoja apate kibali cha kushiriki katika Mkutano huo muhimu.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kuwa katika kipindi hiki cha mapumziko kuelekea Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge wenzetu Waislam watakuwa kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, nitumie fursa hii kuwatakia Mfungo mwema na Sikukuu njema ya Eid El-Fitr.

**Waheshimiwa Wabunge,** baada ya maneno hayo, sasa naahirisha Bunge mpaka tarehe 8 Aprili, 2025 Saa 3:00 Asubuhi kama ilivyotamkwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**

Dkt.Tulia Ackson (Mb)
**SPIKA**

14 Februari, 2025